East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature

OPEN ACCESS

*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya

Volume-8 | Issue-9 | Sep- 2025 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2025.v08i09.006

**Original Research Article**

# Mchango wa Upeaji wa Utambulisho Katika Diskosi za Wabunge Wanawake Kuhusiana na Mamlaka Katika Bunge la Taifa la Kenya

Nkanga Misheck[1], Dkt. Micheni Mutegi Ph.D[2*], Dkt. Mwembu Kimathi, Ph.D[2]

[1]Chuo Kikuu cha Tharaka, S. L.P. 20– 60215, Marimanti, Kenya
[2]Chuo Kikuu cha Tharaka, S. L.P. 193– 60215, Marimanti, Kenya

**Article History**
**Received:** 04.07.2025
**Accepted:** 02.09.2025
**Published**: 13.09.2025

**Journal homepage:**
https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Diskosi za kisiasa za wanawake zina mchango muhimu katika kuthibiti mamlaka katika jamii ambayo imetawaliwa na wanaume. Kupitia uchunguzi wa lugha, utambulisho wa mwanasiasa na ushirika wake kwa vikundi maalumu unaweza kujitokeza kupitia upeaji wa kiutambulisho. Utafiti huu umechunguza mchango wa upeaji wa utambulisho katika diskosi za wabunge wanawake kuhusiana na mamlaka katika Bunge la Taifa la Kenya. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uchanganuzi wa Peo na mtazamo wa Uchanganuzi Hakiki-Makinifu wa Usemi. Nadharia hizi zilitumika kutathmini mchango wa upeaji wa utambulisho kwenye diskosi za wabunge wanawake wakati wa kuunda utambulisho kuhusiana na mamlaka. Chanzo cha data ya utafiti huu ilikuwa video ambazo zilikuwa zimehifadhiwa katika mtandao wa *YouTube,* kutoka kwa hotuba za wabunge wanawake 169, waliochaguliwa na wapiga kura katika bunge la 11, 12 na 13 la taifa la Kenya. Wasailiwa walikuwa wanawake 111 waliochaguliwa kuwakilisha kaunti pamoja na wanawake 58 waliochaguliwa kuwakilisha maeneobunge mbalimbali katika Bunge la Taifa. Mbinu ya utafiti iliyotumika kukusanywa data ilikuwa utazamaji na usikilizaji wa sauti ninga kutoka kwa mtandao ya *YouTube*. Utafiti huu umebaini kuwa. upeaji wa utambulisho huwa na dhima zifuatazo: dhima ya kudumisha mamlaka ya jinsia ya kike dhidi ya mabadiliko, kukarabati hali ante kwa njia ya kupanua wa mamlaka na kubadilisha mahusiano ya mamlaka yaliyopo baina ya jinsia.

**Keywords:** Diskosi, Jinsia, Mamlaka, Peo ya utambulisho, Upeaji wa utambulisho, utambulisho. Wanawake.

**Copyright © 2025 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1. UTANGULIZI

Mamlaka ni mchakato wa mawasiliano ambapo kundi lenye kuhodhi mamlaka huyadumisha kwa njia na raslimali anuwai (Faiclough 2003; Craig na wenzake 2017). Kundi lenye mamlaka hudhibiti mamlaka yake kupitia makubaliano na kuyadumisha kwa kutumia lugha. Katika masuala ya kijamii na kihistoria, kila jinsia hutumia lugha kwa njia fulani ili kudhibiti mawasiliano baina yao. Kwa mfano, Piece (2003), alidai kuwa jamii imekuwa ikijengwa kwa misingi ya kiubabedume. Hivyo, wanaume wamepata hadhi ya juu kuliko wanawake. Hali ambayo imezua uteuzi na matumizi ya misamiati inayorejelea jinsia kwa mamlaka fulani katika maingiliano ya kijamii. Misamiati hiyo inaonyesha ama kuhusishwa au kutohusishwa kwa makundi fulani katika masuala ya jamii. Kutohusishwa kwa wanawake katika ujenzi wa jamii kumechangia katika kudhalilishwa kwa wanawake kupitia lugha.

### 2. Yaliyoandikwa Kuhusu Diskosi na Jinsia

Utafiti kuhusu jinsia na mamlaka ulifanywa na Kimenyi (1992). Utafiti wake ulionyesha kuwa diskosi za wanawake nchini Rwanda ziliwaathiri wanawake kwa kuwa lugha ziliwapa wanaume hadhi ya juu kuliko wanawake. Utafiti wa Kimenyi (keshatajwa) ulithibitisha kuwa lugha nchini Rwanda imetumika kuwapokonya wanawake mamlaka.

Atango (2010) alifanya utafiti kuhusu tofauti za kijinsia katika bunge la Kameruni. Utafiti wake ulibainisha kuwa kuna tofauti za kijinsia wakati wa mijadala bungeni kwa viwango vya ufafanuzi na ukadiriaji kiasi. Utafiti wa Atango (keshatajwa) ulingamua kuwa, kupitia lugha, wanawake hujengwa na kubomolewa kimamlaka. Utafiti wa Atango (Keshatajwa) umesaidia kutathmini namna lugha hutumika kupanga jinsia kimamlaka kupitia uteuzi wa msamiati maalumu.

***Corresponding Author:** Dkt. Micheni Mutegi
Chuo Kikuu cha Tharaka, S. L.P. 193– 60215, Marimanti, Kenya

Wanawake wamekuwa kimya wakati wa kufanya maamuzi katika jamii na ulimwenguni (Mokebo 2015). Kimya hiki kimesababisha ubaguzi unaochangia kuunda na kudumisha ukosefu wa mahusiano ya kimamlaka kati ya wanaume na wanawake katika viwango vya kimaeno, kitaifa na kimatafia. Utafiti wa Mokebo (keshatajwa) ni muhimu katika kutathmini lugha ya wanaume. Hata hivyo, utafiti huu ulilenga kuangazia diskosi za wanawake ambazo kwa maoni ya Mokebo kilikuwa kikundi nyamavu.

Utafiti uliofanywa na Asige na wenzake (2024), ulichunguza vipashio vya mamlaka katika midahalo ya siasa za uchaguzi wa mwaka 2022 nchini Kenya kwenye jukwaa la kidijitali la *YouTube*. Utafiti huo ulilenga kutambua mchango wa lugha kama chombo kinachodhihirisha mamlaka katika jamii kwa kuchanganua baadhi ya vipashio vinavyodhihirisha mamlaka katika mdahalo wakati wa uchaguzi wa 2022 Nchini Kenya.

**3. Swali la Utafiti**

Upeaji wa utambulisho katika diskosi za wabunge wanawake katika Bunge la Taifa la Kenya una mchango upi wa kutambulisha wanawake na mamlaka?

**4. Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu umechunguza upeaji wa utambulisho katika diskosi za wanawake kuhusiana na mamlaka katika bunge la taifa la Kenya kwa kutumia mtazamo wa Uchanganuzi Hakiki-Makinifu wa Usemi na Nadharia ya Uchanganuzi Peo Mtazamo wa UHMU hulenga kuonyesha uhusiano uliopo baina ya lugha na jamiilugha kimatumizi, ili kufikia malengo ya lugha. Hivyo, husaidia wahakiki wa lugha kupata dhana za kiisimu zinazobainika katika kudhibiti na kubadilisha jamii kupitia ufasiri na uelewa wa matini mbalimbali za vipengle vya kijamii na tamaduni. Nadharia ya Uchanganuzi Peo, vilevile, ilitumiwa ili kuziba mwanya wa upangaji wa tajriba, imani na maoni ya jamii.

**5. Mbinu za kukusanya data**

Utafiti huu umekuwa wa kimaelezo, kiufafanuzi na kiuhakiki. Umetoa ufafanuzi wa hali za kijamii, tajriba, makundi na miktadha ya masuala yanayohusu jamii (Yuane 2005). Umechanganua upeaji wa utambulisho katika diskosi za wabunge wanawake katika bunge la taifa nchini Kenya kupitia ujisawiri na kusawiriwa kwao katika diskosi za wabunge wanasiasa wakati wa kujitambulisha kupitia diskosi zao.

Utafiti huu ni wa kimaktabani. Eneo la utafiti huu ni mtandao wa *YouTube*. Mtandao wa *YouTube* ni eneo ambalo podikasti za video za wabunge wanawake, wakiwa nyanjani na bungeni, wakitangamana na wananchi, zilikuwa zimehifadhiwa kwa njia ya kielektroniki. Jumla ya wabunge wanawake 169, walichaguliwa na wapiga kura katika bunge la kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu.

Utafiti huu ulitumia matini kutoka kwa diskosi za wabunge wanawake 169 kutoka bunge la kitaifa. Idadi hii iliafikiwa baada ya kugawa wanawake katika makundi mawili, kundi la kwanza lilikuwa na wanawake 58 waliochaguliwa kuwakilisha eneobunge, kundi la pili, lilikuwa na wanawake 111 waliochaguliwa kama wawakilishi wa kaunti. Makundi yote yalitathminiwa mihula ya kuchaguliwa, kwa kila mbunge mwanamke katika uchaguzi wa 2013, 2017 na 2022. Baada ya utathmini huo, ilibainika kuwa wanawake 10 walichaguliwa kwa mihula mitatu mfululizo, aidha, wanawake 40 walichaguliwa kwa mihula miwili na wanawake 119 walichaguliwa kwa muhula mmoja pekee (KeWoPA 2013, 2017, 2022). Milroy (1987) alipendekeza matumizi ya sampuli ndogo katika utafiti wa lugha kwa kuwa sampuli kubwa una uwezo wa kuzua data yenye urudufu mwingi.

## 6. MATOKEO

**6.1 Mchango wa Kudumisha Utambulisho wa Kina Mama**

Baadhi ya diskosi za wabunge wanawake zimeonyesha kudumishwa kwa uaminifu katika maingiliano baina ya jinsia tofauti. Kwa mfano, katika hotuba ifuatayo mwanamke anang'ang'ana kudumisha uaminifu zaidi ya makundi mengine kupitia lugha:

**Ht. 1:** Hebu tupitishe mswada huu ili tuinue kina mama wa Kenya. Sote tusimame na wanawake ambao wataamka asubuhi sana kutupigia kura. Ni wanawake pekee ndio hujitolea. *Inasemekana kuwa ikiwa mwanamke atakuhahidi, atakupa*.

Katika Ht. 1, Mbunge mwanamke anajadili mswada wa kuinua akina mama kiuchumi. Katika mjadala huo, mbunge mwanamke anaonyesha umuhimu wa kusimama na kina mama kwa kuwa, jinsia ya kina mama ina sifa maalumu ya kuahidi na kutimiza ahadi, wanapoingiliana na makundi mengine. Mzungumzaji anasema "*inasemekana kuwa, ikiwa mwanamke atakuahidi, atakupa."* Diskosi hii inaonyesha mtazamo wa mzungumzaji kuhusu jinsia ya kike na makundi mengine wanayoingiliana nayo katika jamii. Neno *inasemekana* katika sentensi hii, limetumika kukuza itikadi za kiurejelezi ambazo zinatambulisha wanawake wakati wa maingiliano na makundi mbalimbali katika jamii. Leksia "*inasemekana,* vilevile, inaonyesha mtazamo wa makundi ya jamii kuhusu mwanamke kwa kuwa, inatumika kurejelea wanawake wanapoingiliana na makundi mengine kwa peo za kuahidi na kutimiza ahadi zao. Leksia *inasemekana*, imetumika kuonyesha utambulisho wa jadi wa kuahidi na kutimiza ahadi miongoni mwa wanawake. Sifa hii, aidha, imedumishwa miongoni mwa wanawake katika jamii na imetumika kutambulisha wanawake wanapoingiliana na makundi mengine.

Mahusiano kati ya mwanamke na makundi mengine yanadumishwa kupitia viambishi nafsi *a* na *ku* katika neno *a*ki*ku*ahidi *a*ta*ku*pa. Kiambishi "*a"* katika

neno "akikuahadi" na "atakupa" kinatumika kurejelea mwanamke. Huku kiambishi *ku* kikitumika kurejelea muahidiwa. Viambishi hivi vinatambulisha uhusiano wa msemaji na kundi lake kama kikundi kinachoweka ahadi kwa makundi mengine na kuitimiza. Mahusiano yaliyopo baina ya wanawake na makundi mengine, yamedumishwa kupitia itikadi inayokuzwa na leksia *inasemakana.* Mzungumzaji kupitia sentensi, *inasemekana kuwa mwanamke akikuahidi atakupa,* anatambulisha wanawake na sifa ya kutimiza ahadi. Sifa ambayo inastahili kifidiwa na wabunge kwa kuunga mikono mswada wa kuinua kina mama.

Kwa upande mwingine, mbunge mwanamke anajitambulisha kwa peo za kudumisha mipaka ya kikazi. Kwenye hotuba inayofuata, mbunge anatetea nafasi yake dhidi ya kuingiliwa na kundi lisilo la jinsia yake, katika uwakilishi wa wanawake. Mbunge wa kike anaonyesha msimamo wake na msimamo wa makundi shirikishi kuhusu uwakilishi wa wanawake. Hivyo, anasawiri wabunge wanawake kama jinsia iliyo na jukumu la kuwakilisha kina mama kikamilifu pasi na kuingiliwa na watu wengine, wasio wa kikundi chao. Katika Ht. 2 mwanamke anasema.

**Ht. 2:** *Uliposema kina mama wengi watapanguzwa machozi- uliingilia kazi yangu ya kina mama. Mimi mwaka wa 2017 nitatafuta hii kiti yangu ya kuwakilishi wanawake.*

Katika hotuba hii, mbunge mwakilishi wa kaunti anapigania kudumisha nafasi yake ya kuwakilisha kina mama. Mzungumzaji anatumia kauli "*uliingilia kazi yangu ya kina mama"* kuonyesha kuwa, kuna mipaka ya kikazi baina yake na mbunge wa eneobunge la Garisa Township na mwakilishi wa kike. Kauli yake ililenga kuonyesha kuwa mipaka ya kikazi iliyopo kati yake na mbunge wa kiume inafaa kutambuliwa na kudumishwa. Kwa mujibu wa mzungumzaji, kauli ya mbunge wa kiume kuwa "*kina mama watapanguzwa machozi,"* ilikiuka mipaka ya kikazi, hivyo, iliingilia kazi ya mwakilishi wa kaunti. Kauli hii ilionekana kudunisha mamlaka ya mbunge mwanamke kwa kuwa, lengo la matamshi hayo linalenga kudunisha majukumu ya mbunge wa kike.

Kuhusu kujifasiri na kufasiri wengine kama kundi tofauti katika maingiliano, Lichtenstein na Eilders (2019), wanasema kuwa, upeaji wa utambulisho huonyesha uhalisia wa mahusiano kupitia uteuzi na upangwaji wa maneno kwa utaratibu na kwa njia inayoweka wazi kusudi la msemaji. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, matumizi ya leksia *"uliingilia"* katika muktadha wa *uliingilia kazi yangu,* yanaweka bayana kusudi la mbunge wa kike, kuwa mbunge wa kiume alivuka mipaka ya kikazi na kuingilia kazi za kikatiba ya kundi la kina mama. Kauli hii, aidha inakuza mahusiano kijinsia na kazi zao. Inaonyesha kuwa, kuna tofauti ya kikazi kati ya mwakilishi wa kina mama na mbunge wa kiume. Matamshi ya mzungumzaji yalilenga kuonyesha mipaka ya kazi ya kila mtu. Mipaka hiyo inalindwa ili kudumisha mamlaka ya mbunge mwanamke dhidi ya kuingiliwa na makundi mengine.

Peo ya utambulisho inadumisha kuwa, mbunge wa kike ana jukumu la kuwakilisha wa jinsia ya kike pekee, huku, mbunge wa kiume akitarajiwa kushughulikia na masuala ya eneobunge lake. Dhima ya hotuba hii ni kudumisha mipaka ya kikazi na kukuza utambulisho wa mbunge wa kike kama mwanakikundi anayetetea masuala ya wabunge kina mama katika kazi zao. Kwa mujibu wa mzungumzaji, masuala ya wanawake serikalini yanafaa kulindwa na mwakilishi wa kike wala si makundi mengine. Aidha uwakilishi wa wanawake katika kaunti husika haufai kuingiliwa na wanaume anayepigania kiti cha ubunge. Upeaji wa utambulisho katika diskosi hii unatambua kuwa kazi ya mbunge mwanamke ni kuwakilisha kina mama pekee, vilevile, haifai kwa kuwa mipaka ya kikazi inastahili kudumishwa.

Vilevile, mahusiano ya jinsia yanadumishwa kazini haswa, ndani na nje ya bunge. Hivyo, wabunge wa kike na wa kiume wanajisawiri kama jinsia inayojengana na kukamilishana. Katika baadhi ya diskosi, wabunge wanawake wanatetea miswada inayochangia kuwepo kwa ushirikiano wa jinsia, ambapo, jinsia zote zinaishi kwa kujengana na kikamilishana katika kazi zao. Hali hii inathibitishwa wakati mzungumzaji anasema kuwa *wanawake pekee yao hawawezi kufanya kila kitu,* katika hotuba inayofuata:

**Ht. 3:** Mswada huu unalenga, bila shaka, kushirikiana na kanuni wazi zilizoelezwa kikatiba, pamoja na kuweka wazi sauti ya wanawake. *Wanawake pekee yao hawawezi kufanya kila kitu*. *Vilevile wanaume*. Tunahitaji wanaume, sio kwa bunge hili pekee hata nje ya bunge. Sawa na hili, wanaume pia wanatuhitaji katika bunge hili na hata nje ya mbunge. Hili ni suala ya maingiliano sawa.

Katika Ht. 3, mzungumzaji anatetea ushirikiano baina ya jinsia ya kiume na kike katika utendakazi wao. Mazungumzo ya mbunge yanalenga kukashifu mtazamo wa jinsia moja kutoshirikisha jinsia nyingine katika shughuli za bunge, ndani na nje ya bunge. Maneno ya mzungumzaji yanaonyesha umuhimu wa kutagusana baina ya wanawake na wanaume wakati wa kazi. Mahusiano ya kijinsia yanafaa wakati wa kufanya kazi, kwa kuwa, jinsia moja haiwezi kufanya kila kitu. Gordon na wenzake (2015) wanatetea kuwa jinsia hujigawa kimajukumu kwa misingi ya kuwa kiume au kike, hivyo, kila jinsia huwa na kazi inayotambulishwa kwayo. Kuendelezwa kwa kazi za jinsia bungeni na nje ya bunge ni njia moja ya kujengana na kukamilishana kimajukumu baina ya jinsia. Hali hii inaendelezwa na kudumishwa kwenye diskosi za wabunge wanawake wakati mbunge mwanamke anaposema; *Wanawake pekee yao hawawezi kufanya kila kitu*. *Vilevile wanaume*.

Kwa upande mwingine tajriba ya jamii ya kugawa jinsia kimajukumu, inazidi kudumishwa wakati wabunge wanarejelea ufaafu wa kila jinsia kushughulika na kazi yao kila wakati. Utambulisho wa jinsia kwa aina hii, inadumisha mahusiano ya jinsia kimajukumu na kuendeleza mahusiano hayo katika shughuli za kila siku. Peo ya kiutambulisho katika diskosi hii, inaonyesha ufaafu wa kila jinsia katika kuendeleza majukumu yao ya kijinsia kwa kupinga hatua za kijamii na kisiasa za kupendelea jinsia moja na kuiachia jukumu la kufanya maamuzi ya kila kitu.

### 6.2 Mchango wa Peo za Utambulisho Katika Ukarabati wa Mahusiano ya Mamlaka

Ukarabati wa jamii ni uhawirishaji upya wa taratibu za jamii kwa kushirikisha mabadiliko ya taasisi za kijamii, tabia za wanajamii na mahusiano baina ya wanajamii (Wilterdink na Form 2024). Aidha, wataalamu hawa wanadai kuwa, ukarabati wa masuala ya kijamii, huchangia kuunda jamii mpya. Wakishughulikia suala hili Fox na Oxley (2003) wanasema kuwa wanawake wanaangazia masuala fulani ya kijamii yanayohusu wanawake, kama vile: masuala ya ndoa, kuavya mimba, elimu kwa wasichana na mambo mengine. Masuala haya huwa ni kigezo za kutambulisha wanasiasa kijinsia. Kwa upande mwingine, Shapiro (1985) alibainisha kuwa masuala yanayohusishwa na jinsia ya kiume aghalabu hugusia nyanja za kiuchumi, masuala ya polisi na kijeshi, makosa ya jinai, siasa na biashara.

Ukarabati wa masuala ya jamii hutokana na sababu kadhaa: zikiwemo maingiliano baina ya makundi tofauti ya jamii, mabadiliko ya kiekolojia kama vile kugunduliwa kwa maliasili, kutokea kwa magonjwa na mabadiliko ya teknolojia. Mabadiliko, aghalabu, hutoka kwa kundi ndogo la kijamii na huchochewa na itikadi, hali za kiuchumi pia vuguvugu za kisiasa. Mabadiliko hayo baadaye huathiri mifumo ya jamii nzima kwa kuwa athari zake hubaki katika jamii. Baadhi ya mabadiliko yanaonekana katika diskosi za wabunge wanawake, ambapo diskosi zimeonyesha kuwa ukarabati umefanya kwa njia masuala mbalimbali kuhusiana na jinsia ya kike.

#### 6.2.1 Kukarabati kwa Kupinga Mahusiano ya Utambulisho wa Kiunyanyapaa

Baadhi za peo za utambulisho zinaonyesha hali ya unyanyapaa wa kijinsia hasa wakati wanasiasa wa kiume wanatambulisha wabunge wenzio wa kike kwa leksia zinazosawiri mtazamo wa umbo la mwili pamoja na kuwahusisha na majukumu ya familia. Taswira ya unyanyapaa inajitokeza kwenye umbo la mtu binafsi na kuendelezwa kwa taasisi nzima (Marini na Brinton 1984). Kwenye baadhi ya dondoo, umbo la wanawake linatumika kama kipimo cha kutambulisha wanawake bali si kazi na taaluma zao (Yieke 2002). Akiunga mkono mtazamo huu, mzungumzaji anasema hivi katika Ht. 4 na Ht. 5 mtawalia:

**Ht. 4:** Kwa kweli namshukuru sana Mhe. Rais kwa kumteua mwanamke, na si mwanamke tu, bali ni mwanamke ngangari kutoka Kandara, Muranga. Naona wanawake ngangari wengine wanazidi kujitokeza. Nataka kuhimiza dadangu kuwa kazi hii ni ngumu. *Majina ambayo wanawake wamekuwa wakiitwa, yakome***.** Nchi lazima ikumbatie na kukubali wanawake kama viongozi wa kiwango sawa, uzito na busara ili tuweze kuwahudumia watu kwa kiwango kinachotoshana chini ya sheria katika jamii kama binadamu wanaotoshana.

**Ht. 5:** Tunahitaji kutafuta majina ya kuita wanaume wanaotuita slayquens na flower girls. Nafikiri kuwa huu ni muda mwafaka wa kusalimu amri majina yote mliyo nayo na kuanza kuheshimu wabunge wanawake, kwa kuwatambulisha kama wabunge. Tutambueni kama wabunge kina mama wala si slayqueen au flowergirls ama kwa kutumia jina lolote lile mtakalo. Sisi sote tumechaguliwa hivyo, tuwe kielelezo ikiwa tunataka kuwa kielelezo. Ikiwa tungependa kuwa kielelezo, hebu tuwe kielelezo cha amani, tuwe kielelezo cha maendeleo na kupiga hatua kwenda mbele…

> *(Tunahitaji kutafuta majina ya kuita wanaume wanaotuita malkia wa mapenzi na mashabiki wa upendo. Nafikiri kuwa huu ni muda mwafaka wa kusalimu amri majina yote mliyo nayo na kuanza kuheshimu wabunge wanawake. kwa kuwatambulisha kama wabunge. Tutambueni kama wabunge wa kina mama wala si malkia wa mapenzi au mashabiki wa upendo ama kwa kutumia jina lolote lile mtakalo. Sisi sote tumechaguliwa hivyo, tuwe kielelezo ikiwa tunataka kuwa kilelezo. Ikiwa tungependa kuwa kielelezo, hebu tuwe kielelezo cha amani, tuwe kielelezo cha maendeleo na kupiga hatua kwenda mbele…)*

Matumizi ya sentensi *majina ambayo wanawake wamekuwa wakiitwa yakome* katika Ht. 4, na *tutambueni kama wabunge wa kina mama wala si malkia wa mapenzi ama kwa kutumia jina lolote lile mtakalo* kwenye Ht. 5, yanaashiria kuwa wabunge wanawake wanakusudia kukarabati utambulisho wa jinsia ya kike kuhusiana na majina yanayodunisha na kuwashushia hadhi. Katika Ht. 5, mzungumzaji anatoa mifano ya majina yanayodhalilisha wanawake kama: *malkia wa mapenzi* na *mashabiki wa upendo.* Urejelezi kwa majina haya unaudhi mzungumzaji na kundi lake kwa kuwa, yanawatambulisha kimapenzi na kwa misingi ya umbo la mwili wala si kazi wanayofanyia jamii. Matumizi ya maneno *malkia wa mapenzi* pamoja na *mashabiki wa upendo,* yametumika kurejelea wanawake kama kikundi kinachojipamba kwa ajili ya mapenzi, hivyo, yanawapa utambulisho kwa mtazamo wa kimapenzi wala si kazi wanazofanya katika jamii.

Matumizi ya virai: *malkia wa mapenzi* na *mashabiki wa upendo* yanaweka mwanamke kwenye muktadha wa mapenzi. Kila yanapotumika, huonyesha

mwegemeo wa kiunyanyapaa kwa kuwa yanatumika kutazamia mwanamke kwa mwegemeo wa kimahusiano ya kimapenzi na mwanamume (Indede 2011). Kwa kuwa utambulisho wa wanawake kupitia virai *mashabiki wa upendo, malkia wa mapenzi* pamoja na majina mengine yanayowatambulisha kama chombo cha mapenzi unamdunisha na kumdhalilisha mbele ya mwanamume, mzungumzaji anasisitiza kuwa, kila mbunge wa kina mama arejelewe kama mbunge. Anataka majina yote ya kiunyanyapaa, yanayotumika kutambulisha mwanamke kwa misingi ya jinsia, yakome. Vilevile anataka wabunge wanawake warejelewe kama wabunge sawa na wenzao wa kiume. Kwa hivyo, kutambulisha wanawake kwa leksia zinazomdhalilisha na kumsawiri kama chombo cha mapenzi kunashusha hadhi ya mwanamke kutoka kiwango cha binadamu hadi mashine (Kibet na Wenzake 2021). Ikiwa wanawake ni chombo cha mapenzi, basi anapaswa kuburudisha mwanamume kwa kumfanya mchangamfu kila mara. Aidha, anafaa kujitengeneza na kujipamba kwa ajili ya mumewe (Indede Keshatajwa).

Kusudi la mzungumzaji ni kuhakikisha kuwa majina yanayotambulisha kina mama kiunyanyapaa, yaachwe ili mwanamke apate mamlaka sawa na mwanamume. Mzungumzaji katika Ht.6, anapinga peo za utambulisho husika kwa kusema:

**Ht. 6:** "*Hatutakubali muwafanye wanawake wanasiasa kuwa vyombo vya mapenzi ili muwe na mkiwatambulisha kimapenzi."*

Kauli yake, inaonyesha kuwa mtazamo wa kiunyanyapaa uliopo, ufanyiwe marekebisho kwa kutafutiwa majina mbadala. Kwa misingi hii, wazungumzaji wote walioshughulikia mitazamo ya kiunyanyapaa kuhusu mwanamke, wanakuza itikadi kuwa mitazamo yoyote yenye miegemeo ya kijinsia na inayotambulisha mwanamke kiunyanyapaa isikubalike na wabunge katika bunge la taifa ya Kenya. Aidha, anapendekeza mabadiliko yatakayochangia kuleta usawa yawepo ili kupinga hali zilizopo pamoja na kupindua mitazamo hiyo (Maeckellbergh 2009). Kwa upande mwingine, diskosi za wabunge wanawake zinaonyesha kuwa mamlaka ya wanawake katika jamii yanafaa kufanyiwa ukarabati unaolenga kupanua utambulisho wao katika ulingo wa siasa na kijamii.

### 6.2.2 Kukarabati kwa Kupanua Utambulisho wa Wanawake

Urekebishaji wa kupanua mamlaka hutokea iwapo taratibu za jamii zinaingiliwa na hali za kawaida (Elias 1991). Kwenye mwingiliano huu, kuna uwezekano wa kundi fulani kuhusishwa kwenye kikundi ili kuchochea kuhalalishwa kwa taratibu za jamii kwa minajili ya kukarabati utambulisho baina ya kikundi (Gordon na Wenzake 2015). Wakati wa kuingiliana baina ya kundi tawala na kundi tawaliwa, kikundi tawala hulenga kupanua mipaka ya mamlaka yao katika jamii na kulazimika kupanga upya jamii kwa misingi ya mila na desturi za jamii. Kwa mfano, katika hotuba ifuatayo mwanamke anahamasisha kuwa sauti ya kina mama isikizwe kila mahali, nyumbani na bungeni, kwa njia sawa na wanaume. Katika Ht. 7, mzungumzaji anasema:

**Ht. 7:** Mswada huu, unalenga kukubaliana na kanuni zilizo wazi za kikatiba na kushirikisha sauti za wanawake kwenye maamuzi. Wanawake pekee yao hawawezi kuendeleza mambo. Vilevile wanaume. *Tunahitaji wanaume si katika bunge hili, hata nje, sawa na sisi, wanaume wanatuhitaji, si katika bunge hili, ila hata nje*, ni suala la kusaidiana kwa pande zote.

Kwenye Ht. 7, mzungumzaji anafafanua nafasi ya kina mama kwa wabunge wenzake. Jukumu la kina mama la kuwajibika kwa kiwango sawa na wanaume linajitokeza kupitia peo za kuwajibika kwa wanawake, bungeni na nje ya bunge, kwa kiwango sawa na wabunge wanaume. Mzungumzaji anasema, *"Tunahitaji wanaume si katika bunge hili, hata nje, sawa na sisi, wanaume wanatuhitaji, si katika bunge hili, bali hata nje.* Maneno haya yanapanua sauti ya kina mama bungeni na nje ya bunge kwa kiwango kinachotoshana na wabunge wanaume.

Upanuzi wa sauti za kila jinsia kwa kiwango sawa unafaidi katika kuleta maendeleo bungeni na nje ya bunge. Kupitia kauli ya mzungumzaji, mwakilishi wa kike anathibitisha na kuhalalisha misimamo ya kikundi cha kina mama na wanaume kuwa, makundi ya kufaana bungeni na nje ya bunge. Kufaana baina ya makundi ya wanaume na wanawake ndio njia ya kupiga hatua kimaendeleo. Kushirikishwa kwa wanawake katika maamuzi ya kila namna, bunge na nyumbani, ni muhimu katika jamii inayoendelea (Elias 1991).

Suala la kijamii hufikia kiwango cha kuhalalishwa ili kufanya jambo lisilokubaliwa kwenye jamii likubalike katika mifumo ya jamii (Gordon na wenzake 2015). Mabadiliko hukubalika kupitia itikadi zilizopangwa na kuwekewa mikakati inayolenga kuunda mtazamo mpya kwa umma. Kupitia Ht. 7, masuala ya wanawake yameshughulikiwa kisheria, ila mapendekezo ya kisheria hayajatimizwa. Mswada ya kisheria unatarajiwa kusaidia katika kushughulikia ushirikishwaji wa wanawake katika kufanya maamuzi. Hali hii inaleta usawa wa jinsia kwa kuhalalisha mamlaka ya kina mama bungeni na hata nje ya bunge. Aidha, peo ya utambulisho kupitia hotuba hii, imetumika kupanua mamlaka ya wanawake katika shughuli za jamii na kisiasa. Katika hotuba inayofuata, diskosi za mwanamke inatekeleza upanuzi wa utambulisho wa wanawake kutoka bunge hadi nyanja mbalimbali za jamii.

**Ht. 8:** Hallo. Yangu ni machache sana, maana siku ya leo ni siku ya mheshimiwa baba yetu. Baba yetu, Mheshimiwa (jina limebanwa). Hallo! Mimi nataka kupeana ahadi yangu kwa Mheshimiwa (jina limebanwa) ya kwamba *mimi* ni mwakilishi wa kina mama wa kaunti ya Makueni. *Pale bunge, *wamama ninawaelewa sana.*

Hakikisho langu ni kwamba, kura za kina mama wa Makueni ni zako. Hallo! *Na ya kwamba mbele ya mwanamke, mbele ya *wamama; wanaume hawana ujanja*. Na kwamba wale mnaona hapa watapatiana kura zao, kwa maana wanawake wataongea na wao…

> *(Habari! Yangu ni machache sana, maana siku ya leo ni siku ya mheshimiwa baba yetu. Baba yetu, Mheshimiwa (jina limebanwa). Habari! Mimi nataka kupeana ahadi yangu kwa Mheshimiwa (jina limebanwa) ya kwamba mimi ni mwakilishi wa kina mama wa kaunti ya Makueni. Pale bunge, kina mama ninawaelewa sana. Hakikisho langu ni kwamba, kura za kina mama wa Makueni ni zako. Habari! Na ya kwamba mbele ya mwanamke, mbele ya kina mama; wanaume hawana ujanja. Na kwamba wale mnaona hapa watapatiana kura zao, kwa maana wanawake wataongea na wao…)*

Hotuba hii inahusu kauli ya mbunge mwanamke kuhusu mahusiano ya wanawake na makundi mengine. Mzungumzaji anajisawiri kama mwanakikundi aliyeelewa uwezo wa kikundi cha wabunge wanawake bungeni, wanapoingiliana na makundi mengine. Anatetea utambulisho wa wanawake, kama mwanakikundi anayeelewa kikundi cha kina mama, aliposema; "*Pale bunge, *wamama, ninawaelewa sana."* Kauli hii inatumika kama hakikisho la mzungumzaji kuwa mwelekeo wa kina mama bungeni unatoshana na mwelekeo wa kina mama wote nyanjani na wakati wa kupiga kura.

Kwa kurejelea Ht. 8, ni wazi kuwa, uelewa wa mzungumzaji, ambao ndio chanzo cha ahadi na hakikisho, ni kwamba kikundi cha wanawake bungeni kina na mamlaka ya juu kuliko makundi ya wabunge wanaume. Kwa sababu hii, mzungumzaji anachukulia kuwa, wanawake, wote ni kikundi kimoja na kina sifa sawa, bungeni na nyanjani. Anatumia peo ya utambulisho kuwa *mbele ya mwanamke, wanaume hawana ujanja* kutambulisha jinsia ya kike na makundi ya watu walio mkutanoni wakiwemo wanaume. Hili ni dhihirisho kuwa, sifa ya wanawake bungeni imepanuka kutoka bunge hadi mashinani kwa wapiga kura.

Suala la uwezo wa kushawishi miungoni wanawake limeshughulikiwa na baadhi ya wataalamu akiwemo Mutiso (1999), ambaye anadai kuwa, wanawake wamekuwa wakitumiwa katika shughuli za kijasusi, ili kuchunguza na kujua siri za mashujaa. Kupitia uwezo wao wa kiushawishi, waliweza kufanikiwa kujua siri za mashujaa na hatimaye kusababisha vifo vyao. Kwa mujibu wa diskosi katika Ht. 8, uwezo wa wanawake wa kushawishi unapanuliwa kushughulikia wapiga kura na wanaume wote hata walio na ujanja. Aidha uwezo huo umepanuliwa kutoka bungeni na kusambazwa mashinani kwa wapigakura na wanaume. Mzungumzaji ametumia tajriba yake bungeni kutathimini na kuelewa uwezo kiushawishi baina ya wabunge wanawake, na kuutumia kutambulisha makundi ya wanawake.

Kama mikakati wa kupanua mamlaka yake na kikundi chake kwa jamii, mzungumzaji anatumia lugha kuhakikisha na kuahidi mheshimiwa (jina lake limebanwa) kuwa, wanawake wana uwezo kushawishi hata makundi ya wanaume wenye ujanja. Machukulio yanayokuzwa na kauli hii ni kwamba, mzungumzaji anasawiri wanawake kama kundi lililo na uwezo wa kufanikiwa kupitia ushawishi. Anahakikishia mheshimiwa (jina limebanwa) kuwa kina mama wangempa kura, vilevile, wangesaidia kushawishi wanaume pia. Matini zilizoteuliwa kama ithibati katika diskosi hii, inatambulisha mzungumzaji kama mmoja wa wanakikundi aliye na uzoefu wa kimaingiliano na makundi mbalimbali ya jamii.

Kupitia Ht. 8, mzungumzaji amepanua utambulisho wa wanawake katika jamii na kuonyesha uchanya wa kuchukulia sauti ya mwanamke kwa uzito licha ya tamaduni zinazokandamiza jinsia ya kike. Mzungumzaji anatambulisha mahusiano baina ya mwanamke, na makundi mengine, kama mahusiano yasiyo na upungufu wa kiushawishi. Mtazamo huo unasawiri kupanuka kwa mamlaka ya mahusiano ya wanawake kutoka bunge na kuyaendeleza katika mazingira tofauti, katika nyanja za kisiasa na kijamii, ili kukarabati wa mahusiano kati ya wanawake na makundi mengine ya jamii.

Mfano mwingine wa ukarabati wa mamlaka unajitokeza wakati mbunge wa kaunti alijitambulisha kama mwakilishi wa watu wote kinyume na uwakilishi wa jinsia ya kike katika Ht. 9, Kwenye hotuba hii, mzungumzaji anakana nafasi yake ya kikatiba, ya kuwakilisha wanawake wa kaunti yake na kupanua mipaka ya uwakilishi ili kujiweka katika nafasi bora ya kujadili ushirikiano kati yake na wakaaji wa kiume kwa kusema;

**Ht. 9:** *Mimi si mwakilishi wa kina mama pekee yake ninawakilisha wanaume, vijana na wazee wote wa kaunti ya Taita Taveta.*

Kikatiba, mwakilishi wa kaunti anajukumikia kuwakilisha kina mama katika kila kaunti nchini Kenya (Katiba 2010). Utambulisho wa aina hii unadokeza kuwa mitazamo ya jamii inayoambatanisha mwanamke na majukumu fulani huangaziwe upya. Kwa kuwa, mbunge wanawake wanataka mipaka ya majukumu ya kina mama ipanuliwe kwa misingi ya mamlaka ya kiofisi waliyo nayo. Vilevile, upanuzi wa mamlaka hutegemee hadhi ya ofisi yake wala na ujinsia.

### 6.3 Mchango wa Upeaji wa Utambulisho wa Kupindua Utaratibu wa Jamii

Lugha katika umbo lake la thamani hujadiliwa kwa misingi ya daraja za kimamlaka. Lugha inaweza kutumiwa na kundi lenye hadhi kubwa kudhibiti kundi

lenye hadhi ndogo katika jamii. Kundi lenye hadhi ndogo, aidha, linaweza kubuni miundo mipya ya kupindua taratibu za jamii na mamlaka (Piece 2003). Kwa mujibu wa Freire (1970), ugunduzi wa taratibu za kupindua miundo ya jamii hubadilisha uwezo, mamlaka na kaida za lugha. Diskosi mbalimbali zimeonyesha mabadiliko kwenye taratibu za jamii kwa njia kadhaa kama inavyojadiliwa katika vijisehemu vinavyofuata.

**6.3.1 Kupindua Taratibu za Jamiii kwa Kukashifu Mawazo Potovu Kuhusu Wanawake**

Baadhi ya diskosi za wabunge wanawake zinakashifu na kukataa mawazo potovu kuhusu kitu au mtu fulani hadharani, mara nyingi kwa njia rasmi. Kukashifu ni kulaani na kukataa kitu kwa njia rasmi (Kamusi ya Kingereza ya Macmillan 2002). Kushutumu, kwa kawaida, hufanywa ili kukabiliana na makosa, ukosefu wa haki au tabia isiyofaa, kwa lengo la kuonyesha kutoidhinishwa kwa jambo. Kukashifu hulenga kuwajibisha watu binafsi na mashirika mbalimbali yanayoendeleza Mawazo potovu (Kenya law 2012). Kukashifu kunaweza kujitokeza kwa aina nyingi kama vile; kupitia kwa kauli, matamshi na hatua za kisheria. Katika hotuba ifuatayo, mbunge mwanamke anakashifu nafasi aliyopewa na jamii kuhusiana na mamlaka na kutaka mabadiliko. Anasema:

**Ht. 10:** *Kuwa mwanamke katika jamii zingine ni tatizo.* Huwezi simama ukasema huna haki ya kumiliki mali kwa sababu watu wanakufikira kwa njia hasi. Wanaume wengine wanakufikiria kwa njia hasi. Hadi wakati watakapouona uongozi wako, hawawezi kukuamini. Wanaume wengine walikuwa wanauliza, "*kwa nini tuchague mwanamke? Atashikaje rungu?* Kwa hivyo, ningewauliza pia, kwa nini niwe na rungu? *Hatuhitaji rungu bungeni.*

Katika Ht. 10, mzungumzaji analenga kukashifu wanaume katika jamii kwa kumpa mwanamke nafasi duni kuhusiana na haki za kumiliki mali na uongozi katika jamii. Kwa mujibu wa mbunge wa kaunti, kigezo cha jinsia kinazingatiwa na kutumika wakati wa kuteua viongozi na katika kumiliki mali katika jamii. Mzungumzaji anasema *"kuwa mwanamke katika jamii zingine ni tatizo"* kisha anashadidia kuwa tatizo hilo linatokana na wanaume kwa kuwa, ni wanaume pekee ndio huwa wanauliza *"kwa nini tuchague mwanamke, atashikaje rungu."* Diskosi hii imetumika kisiasa, kwa lengo la kukashifu kundi nje (wanaume) ambalo lina miegemeo ya kiubaguzi.

Tendo la kukashifu linatumiwa kuangazia masuala ya kijamii, kisiasa na kimaadili. Wale wanaokashifu huchochewa na tamaa ya haki, usawa na uadilifu. Tendo la kukashifu ni njia yenye nguvu ya kuondoa matumizi mabaya ya mamlaka na ubaguzi wa binadamu katika taasisi. Ingawa kushutumu kunaweza kuzua mjadala, ni njia bora inayotumiwa na watu binafsi pamoja na jamii kutoa hoja zao na kutetea kile wanachoamini kuwa bora. Katika Ht. 10, diskosi imetumika kimkakati ili kufanya kampeni dhidi ya kubaguliwa kwa wanawake katika siasa. Kwa mfano, baadhi ya wasomi hutumia kirai tenzi "kukosewa heshima," wanaporejelea kauli zinazoudhi (Culpeper 2011). Wakati mwingine semi hasi, aghalabu, huenda kinyume na matakwa ya jamii na umma. Hivyo, kuonekana kupendelea mikakati ya kimaksudi ya kutambulisha kundi nje kwa njia ya kupinga mitazamo inayobagua kundi-ndani. Kwa mujibu wa Wodak (2007) wakati ujumbe unawasilishwa kwa njia ya kupinga hali iliyoko, aghalabu, ujumbe huo huchukuliwa kuwa dhabiti na kweli.

Kwa mujibu wa Ht. 10, mwanamke anadunishwa katika shughuli za uongozi wa jamii yake. Mzungumzaji anasema kuwa, wanaume hutaka kujua sababu ya kuchagua mwanamke, kwa kuwa, hana uwezo wa kushika rungu. Anasema; "*wanaume wengine walikuwa wanauliza*, *kwa nini tuchague mwanamke? Hatashikaje rungu?"* Haya ni maswali ya balagha. Maswali haya hubeba itikadi kuwa mwanamke hawezi kushika rungu. Katika jamii za Kiafrika "rungu" ni ishara ya mamlaka na huonyesha hadhi ya mtu katika jamii. Inaweza kurithishwa kutoka kwa kiongozi hadi kwa mtoto wa kiume katika jamii, kama ishara ya kukabidhi mamlaka kwa kijana mwanamume (Momanyi 2018). Kwa hivyo, katika jamii za kiafrika, rungu ilitumika kutambulisha uongozi wa wanaume wala haikuhusishwa na wanawake.

Itikadi inayokuzwa kupitia kauli *"atashikaje rungu?"* ni kwamba wanaume wana shaka kuhusu uwezo wa mwanamke wa kushika "rungu." Katika jamii zingine, mwanamke hana haki ya kumiliki kitu na hana uwezo wa kuongoza jamii. Itikadi za aina hii zinadunisha mamlaka ya wanawake katika uongozi. Kwa sababu hii, utambulisho wa mwanamke kwa misingi ya kutoweza kuongoza, unapingwa na mzungumzaji aliposema "*hatuhitaji rungu bungeni."* Kauli *hatuhitaji rungu bungeni* inaonyesha kejeli kwa mtazamo hasi kuhusiana na uongozi wa mwanamke katika jamii. Kauli hii inaonyesha kuwa taratibu zinazodhalilisha mwanamke zinapingwa na wabunge wanawake bungeni kama inavyoonekana kupitia Ht. 10. Kwa kuwa ni wazo potovu kuhusu wanawake na uongozi wa jamii.

Katika hotuba ifuatayo, mwanamke ameshutumu mawazo potovu kuwa mwanamke aliyeolewa katika eneo ambalo yeye si mzaliwa halisi wa eneo hilo, hafai kuomba kura kama asilia. Kauli ya askofu mmoja aliyetambulisha mbunge mwanamke kama "mwizi wa kura" inasutwa huku mbunge wa kike akidai kuwa kila mwanamke ana haki sawa na mwenyeji asilia wa Thika. Suala la aina hii ni la kiubaguzi. Suala la ubaguzi wa jinsia ni sugu katika baadhi ya nchi kwa kuwa limechangia kuwepo kwa vita vya kijinsia baina ya wanawake na wanaume (Seo na Hollingsworth, 2022). Mzungumzaji anasema yafuatayo katika hotuba Ht. 11.

**Ht. 11:** So, *mtu anakuja kupiga kifua kuwa yeye ndiye wa Thika, sisi ni ndio wa wapi?* Sisi ni wa Thika. Tunalala Thika, tumebarikiwa Thika, tunafanya biashara Thika. Kama Abrahamu aliambiwa, ondoka nitaenda kukubalikia Kanani, pia sisi *Kanani yetu ni Thika na hatutoki. Hatubanduki*. We are here to stay. Na yule mtu anatuona anasikia vibaya, ataendele kuhisi kinyongo. Hatuhami na hatupangwingwi. I want to say, wale wanaelewa; hii Thika, hii Juja na hii Ruiru, the 42 tribes of Thika, Ruiru na Juja huwa wanaishi huku. Usianze hate speech ya kufukuza watu wengine. Usianzie kutenga sisi na wale. Sisi wote ni wanathika.

Katika Ht. 11, mwanakikundi ambaye anatambulishwa kama *yeye* ana mtazamo hasi kuhusu mbunge wa kike aliyechaguliwa katika eneo ambalo si mwenyeji asilia. Matamshi ya mwanakikundi anayetambulishwa kama *yeye* ni ya kudunisha wanawake walioolewa maeneo mengine mbali na kule walikozaliwa. Kikundi cha kina *yeye,* kinachukulia kuwa, kundi la wanawake linalopata uongozi ugenini, ni wezi wa kura za wakaaji wa asilia. Utambulisho wa aina hii kutoka kwa wapinzani wa mbunge mwanamke, unadhalilishwa mwanamke aliyeolewa ugenini, kwa kumtenga mbali na wakaaji asilia wa eneo maalum. Kwa sababu hii kundi la kina mama, linalotambulishwa kwa peo ya wageni, linang'anga'na kupata utambulisho sawa na wenyeji wa maeneo walioolewa.

Kupitia Ht. 11, mzungumzaji anateua kiwakilishi nafasi *sisi* kupinga mpinzani kwa kujitambulisha na kikundi. Anatumia katika sentensi *sisi ni wa wapi?* Kupinga mtazamo wa mwanakikundi nje, haswa mpinzani wake. Mpinzani, aidha anajishirikisha na wasikilizaji baadala ya kujitambulisha kibinafsi. Hali hii inampa nafasi bora ya kujitetea kama mgeni katika hadhira iliyo na mchanganyiko wa wenyeji na wageni. Vilevile, anapinga mtazamo wa mpinzani, *yeye,* wa kugawa watu katika makundi ya wenyeji na wageni katika eneo bunge la Thika Township.

Mzungumzaji anatumia mbalagha *sisi ni wa wapi?* Kushirikisha umma katika kutafuta jibu. Kauli hii inaweka mzungumzaji pamoja na umma katika upande moja wa kutafuta jibu kuhusu makao yao kama kikundi kilichotengwa. Ili kusistiza kuhusu ubora wake kutokuwa mwenyeji, mzungumzaji, aidha, anajilinganisha na Abrahamu aliyeambiwa na Mungu aondoke kwenda Kanani akapate baraka. Peo ya utambulisho kuwa mzungumzaji ni sawa na Abrahamu, zinatumika kukosoa mtazamo potovu kuhusu "uchikwao" wa mwanamke aliyeolewa katika eneo la jamii ambalo, yeye si mzaliwa asilia. Lengo la mzungumzaji ni kukashifu mtazamo potovu kuhusu mwanamke, linanuia kubadilisha mtazamo wa kundi la *yeye,* na wengine walio na mtazamo kama yake, kuhusu uwezo na njia za kutwaa uongozi serikalini.

Mzungumzaji vilevile, ametoa onyo kupitia lugha, kama mikakati ya kudumisha utambulisho wake na kikundi chake. Aidha, amelenga mpinzani na kumwonya dhidi ya kuanza matamshi ya chuki na kutenga watu katika makundi ya wageni na wenyeji; aliposema *"usianze matamshi ya chuki ya kufukuza watu wengine. Usianzie kutenga sisi na wale.* Kauli hii inatolewa kama onyo, kwamba kitendo cha uchochezi ni zao la matamshi ya chuki, na kinaweza kusababisha uhasama kati ya makundi ya wageni na wenyeji. Matamshi ya mzungumzaji yanalenga kukashifu na kubadilisha peo ya utambulisho inaodunisha wanawake. Kwa upande mwingine diskosi za wanawake inachangia kubadilisha utendakazi wa kina mama kwa kusifia utendakazi wao kama inavyojadiliwa katika sehemu ya 6.3.2.

### 6.3.2 Kubadilisha Utambulisho wa Kina Mama kwa Kusifia Utendakazi

Katika hotuba ifuatayo, mzungumzaji analenga kubadilisha utambulisho wa wanawake kwa kuonyesha ubora wa jinsia ya kike katika uongozi ikilinganishwa na uongozi wa makundi mengine. Kupitia njia ya kusifia, msemaji hujipa sifa chanya, hivyo, huonekana kama kielelezo katika jamii (Smith 2000). Mzungumzaji anasema:

**Ht. 12:** Nakushukuru mwenyekiti na inahitaji ujikaze. Ninaposema ujikaze, sisemi kuwa unafanya vibaya, lakini unafanya vizuri sana isipokuwa kama nilivyosema jana, *"kamati zinazoongozwa na wanawake zinazidi kufanya vyema"* Naona (wanaume) mnataka kukashifu hilo. Mnafanya vizuri kwa kamati zenu ila kamati zinazoongozwa na wanawake zinafanya bora zaidi.

Katika Ht. 12, mzungumzaji anasifia utendakazi wa jinsia kike katika kamati za bunge kwa kuulinganisha na utendakazi wa wanaume bungeni. Anaonyesha kuwa, makundi ya kina mama yanayoongoza kamati za bunge, yanafanya vyema kuliko uongozi wa makundi mengine haswa kundi la kiume. Kwa mujibu wa mzungumzaji viongozi wanawake wanaoongoza kamati za bunge vyema wakilinganishwa na wenzio wa kiume. Anathibitisha hili kwa kusema "*mnafanya vizuri kwa kamati zenu ila kamati zinazoongozwa na wanawake zinafanya bora zaidi".* Ubora wa utendakazi wa wanawake unakuzwa na matumizi ya kirai elezi *bora zaidi.* Kirai Elezi *bora zaidi* kimetumika kuonyesha kiwango cha ubora cha kufanya kazi katika kamati za bunge miongoni mwa kina mama. Kimsingi, upeaji wa kulinganisha kwa kusifia hutumiwa kama njia ya kushughulikia matukio kwa kuyahusisha na matukio mengine kwa misingi maalumu (Deville na Guggenheim (2024).

Ulinganisho unaweza kuegemea kwenye kiwango, mwendo na hali ya kuwa nzuri au baya. Matumizi ya Leksia *zaidi* katika sentensi …*mnafanya vizuri kwa kamati zenu ila kamati zinazoongozwa na wanawake zinafanya bora zaidi*… inatumika kutathmini viwango vya utendakazi wa virejelewa na kuweka wazi hali za virejelewa husika katika msingi wa kiutendakazi.

Ulinganisho, hutumika kuzua hali chanya na hasi kwa virejelewa kwa wakati moja (Chiarcos, Claus, na Grabski 2011). Utambulisho wa mzungumzaji kwa sifa chanya hufafanua mtendaji, matukio na muktadha wa kufanyika jambo kwa njia chanya, vivyo hivyo, huchangia kuleta dhana ya umaarufu na udhaifu miongoni mwa wale wanaotambulishwa kwa wakati sawia (Deville na Guggenhaim keshatajwa).

Utambulisho kwa kusifia utendakazi wa wabunge wanawake unasawiri kina mama kama kundi lililomiliki malighafi ya uongozi bora. Hali ya kusifia hunuia kuweka wanakikundi katika hali inayokubalika na jamii kwa hivyo, utambulisho kwa peo za kusifia unalenga kubadilisha mtazamo hasi kuhusu uongozi wa kina mama katika masuala ya mamlaka, kwa kukuza uchanya wa matendo yao katika miktadha ya utendakazi wao bungeni. Aidha, unaonyesha udhaifu wa kundi nje katika uongozi wa kamati za bunge.

**Ht. 13:** *Nataka kumhakikishia tena kuwa*, wanawake wanachangia pakubwa na wana nafasi muhimu nchini. Wana nguvu ya kiidadi. Kwa hivyo, wanawake wa kaunti hii na nchi hii wako wana nafasi bora ya kubadilisha hali ya kisiasa kwa njia yoyote watakayochagua. Na ninajua kuwa, wanawake wanaweza kufanya maamuzi mazuri ya nchi hii, kwa *kuwa tuna mamlaka ya kutunza, na ukiwa na mamlaka ya kutunza, unatakia familia yako mema*. Kwa hivyo, maamuzi ambayo tumeazima kufanyia nchi hii, yatakuwa na manufaa kwa watoto, familia, jamii na mwishowe nchi hii.

Katika Ht. 13, mzungumzaji anasifia uwezo wa wanawake wa kuendeleza watoto, familia, jamii na nchi kupitia uwezo wa kutunza, ambao umemilikiwa na kila mwanamke (Indede 2011). Mtazamo wa mbunge mwanamke kuhusu uwezo wa kutunza wa wanawake ni kuwa, 'uwezo wa kutunza' ni muhimu wakati wa kufanya maamuzi ya kaunti na nchi. Kwa hivyo, ikiwa wanawake wangetumia uwezo huo, pamoja na idadi yao, wangepata nguvu ya kufanya mabadiliko ya hali ya kisiasa katika kaunti na nchi.

Kupitia usifiaji, mzungumzaji hulenga kumsifu mtu kutokana na matendo yake kwa kutoa sifa nzuri, vilevile, huweza hukashifu kwa kutoa sifa kinyume, kuumbua, kunyambua, kukosoa na kadhalika (Wamitila 2004). Kupitia Ht. 13, mzungumzaji analenga kuondoa shaka kwa kuhakikishia wananchi kwa mara nyingine kuwa uwezo wa kubadilisha hali iliyoko, kuhusu siasa na wanawake, ni jambo la kufanya maamuzi kutoka kwa kundi la wanawake. Anadai kuwa kundi la wanawake lina idadi ya kutosha ya kufanya maamuzi pamoja na sifa ya utunzaji ambayo inafaa familia na jamii. Kwa mujibu wa mzungumzaji uwezo wa mwanamke wa kutunza familia ni sifa bora ya kufanya mabadiliko katika kaunti na nchi kwa jumla. Mzungumzaji anatambulisha uwezo wa kutunza wa kina mama kama uwezo wa kutakia familia mema" aliposema*;* "*kwa kuwa tuna mamlaka ya kutunza, na ukiwa na mamlaka ya kutunza, unatakia familia yako mema."* Vilevile ametumia leksia *kuhakikisha tena* ili kuondoa shaka kuwa wanawake hawawezi kubadilisha kaunti na nchi kupitia idadi yao na sifa ya utunzaji ambayo ni muhimu kwa familia. Licha ya kuwa sifa ya utunzaji ni muhimu kwa familia inafaa katika kufanya maamuzi ya familia, jamii kaunti na nchi.

## 7. HITIMISHO

Utafiti huu umehitimisha kuwa wabunge wanawake wana majukumu muhimu katika uwanja wa kisiasa licha ya kusawiriwa, na makundi nje, kama kikundi kisicho na mchango wowote wa maana katika siasa. Diskosi za wabunge wanawake zimeonyesha kuwa wanawake hutazama jambo kwa mtazamo tofauti na wanaume. Kwa misingi hii, sauti ya wanawake ni muhimu katika kufanya maamuzi. Mbunge mwanamke anadai kuwa "Tunahitaji wanaume si katika bunge hili, hata nje, sawa na sisi, wanaume wanatuhitaji, si katika bunge hili, ila hata nje, ni suala la kusaidiana kwa pande zote." Aidha, kwa kiwango kikubwa lugha imechangia katika kudumisha mamlaka, kubadilisha utambulisho wa wanawake na kukarabati hali mbalimbali kuhusiana na utambulisho wa wanawake.

## MAREJELEO


- Asige, E. Saloojee, G. Wanjala, G. Andrews, C. Namagand, H. Mwesige, A. Damiano, L. na Forssberg, H (2025) Participation in activities of daily living after the Akwenda Intervention Program for children and young people with cerebral palsy in Uganda: A cluster-randomized trial: *Developmental Medicine & Child Neurology* Vol; 67, (9)
- Chiarcos, C., Claus, B. na Grabski, M. (2011) *Salience: Multidisciplinary Perspectives on Its Function in Discourse*. Berlin: Walter de Gruyter Craig na wenzake 2017).
- Culpeper, J. (2011). Impoliteness: Using Language to Cause Offence. Cambridge: Cambridge University Press
- Elias, N., (2010) The Civilizing Process: Sociogenetic and Psychogenetic Investigations - An overview and assessment. *History and Theory* Vol 49 Issue 3: page384-411. Doi:10.2307/40864499
- Fairclough, N., (2003) Analysing Discourse: Textual Analysis for Social Research / N. Fairclough. Lancaster University
- Freire, P. (1970). Pedagogy of the Oppressed. New York: Seabury Press.
- Gordon W., Shonin, E., & Griffiths, M. (2015). Mindfulness in psychology: A breath of fresh air? The Psychologist 28(1):28-31
- Hollingsworth, J. &Seo, Y. (2022). How feminism became a hot topic in South Korea's presidential election. CNN. https://www.cnn.com /2022/03/08 Asia/South-Korea election-young-people-intl- hnk-dst/index.html

- Http//: www. KeWoPa.org/wp-content/upload/202/23/ KeWoPA strategic-plan
- Indede, F., (2011) Mwanamke Angali Tata Katika Ushairi wa Kisasa. *Academic Journal. Swahili forum 18 (2011)*-163-197
- Joe Deville, J. Guggenheim, M. & Hrdličková Z. (Eds.) (2016) Practicing Comparison: Logics, Relations, Collaborations. Manchester: Mattering Press. Science & Technology Studies 29(2):74-76; DOI:10.23987/sts.57954 199 pages
- Kibet, J., K., Omollo, R. W. Mavisi, R. (2021) Taswira ya Mwanamke katika Kipindi cha Bi. Msafwari Runinga ya Citizen Nchini Kenya. Chuo kikuu cha Catholic. Doi.org/10.37284/eajss.3.1.430
- Kimenyi, S., & Mbaku, J. (1992) Rents, military elites, and political democracy European Journal of Political Economy*;* Vol; 11, (4) pp: 699-708.
- Lichtenstein, D & Eilders, C. (2019). EU identity frame *EU Identity, Identity Frame, EU, European Union, Comparative research internation.* http;//doi.org/10.34778/2zi
- Maeckellbergh, M. (2009). The Will of the Many: How the Alterglobalisation Movement is Changing the Face of Democracy
- Momanyi, C. 2001) Mamlaka Na Itikadi Katika Nyimbo Teule Za Taarab Tasnifu ya M.A [Haijachapishwa]. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mwangi, S. (2008) Gender Policy and the Impact of Women Involvement in Politics. In Thundu Kiaga A.M. Mwangi S. (Eds) *Assessing Gender Politics in East Africa Region.* Nairobi: DPMF.
- Smith, R. (2000) Assimilative and contrastive emotional reactions to upward and downward social comparisons. In J. Suls L. Wheeler (Eds.), *Handbook of social comparison: Theory and research (pp.*173 -200). New York: Plenum
- The New Constitution of Kenya (2010), Government printer, Nairobi, Kenya.
- Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia. Focus publishers, Nairobi
- Wodak, R. (2007). Language in Ideology. *Journal of Language and Politics 6 (1)*, 1-6.
- Yuane, I. (2005) Cross-Sectional, Descriptive Design, A Qualitative Research, PAACE. *Journal of Lifelong Learning.* 4, 50-60.


**Cite This Article:** Nkanga Misheck, Dkt. Micheni Mutegi, Dkt. Mwembu Kimathi (2025). Mchango wa Upeaji wa Utambulisho Katika Diskosi za Wabunge Wanawake Kuhusiana na Mamlaka Katika Bunge la Taifa la Kenya. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 8*(9), 476-485.